
## KIPIMO KINACHOONESHA KUSHUHUDIA NA KUHUSISHWA KWA WATOTO KWENYE UKATILI MAJUMBANI

**Sehemu ya Kwanza**

a. Kila swali lina sehemu mbili.
b. Kuna machaguo manne katika kila swali.

- Kwanza jibu swali linalouliza ni mara ngapi kumetokea kitendo cha kuumiza mwili au hisia za mama yako au kumfanya ajisikie vibaya, kwa kuweka tiki katika jibu lako
- Halafu weka tiki (√) kuonesha majibu yote yaliyokusaidia kujua nini kilitokea.
- Kama jibu lako likiwa “haijawahi kutokea” katika sehemu ya kwanza, ruka sehemu ya pili ya swali na uendelee na swali linalofuata.



**Kwa mfano:**
**Ni mara ngapi kumekuwa na ugomvi shuleni kwenu?**

**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

**Kama umeweka tiki katika chaguo la “haijawahi kutokea” , endelea na swali linalofuata**

**Ulijuaje?**

☐ Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuamua ugomvi)
☑ Nilisikia kuhusu ugomvi huo baada ya kuwa umetokea.
☐ Nilisikia kuhusu ugomvi huo wakati unatokea
☑ Niliuona ugomvi huo kwa mbali wakati unatokea
☐ Niliushuhudia ugomvi huo kwa karibu wakati unatokea

1. Imewahi kutokea mara ngapi kwa watu wakubwa ndani ya familia yenu kutokuelewana?

**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara Nyingi** | **Kila siku**


Kama umeweka tiki katika chaguo la “haijawahi kutokea” , endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
☐ **Nilisikia baada ya kutokuelewana kwao kutokea.**
☐ **Nilisikia wakati kutokuelewana kwao kunatokea**
☐ **Nilisikia kwa mbali wakati kutokuelewana kwao kunatokea**
☐ **Nilishuhudia kwa karibu wakati kutokuelewana kwao kunatokea**

2. Imewahi kutokea baba yako amemfanya mama yako ajisikie vibaya kwa kumuambia maneno machafu, matusi, kusema kwamba angemfanyia kitu kibaya, kumfokea,kuongea naye kwa hasira au kusema kwamba angemuumiza kwa kutumia silaha kama panga?

Taja kitendo kingine cha kumfanya mama yako ajisikie vibaya…………………………..



**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea" ,endelea na swalilinalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kumfanya ajisikie vibaya baada yakuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati alipokuwa akimfanya ajisikie vibaya**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimfanya mama ajisikie vibaya**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimfanya mama ajisikie vibaya**

3. Ni mara ngapi baba yako amewahi kumkataza mama yako kufanya kitu alichotaka kufanya au kumfanya ashindwe kukifanya? Kama kuondoka nyumbani, kumuona daktari, kutumia simu, kuwatembelea rafiki zake au ndugu?

- Taja kitu kingine ambacho baba yako humkataza mama yako kufanya au kumfanya ashindwe kukifanya…………..


………………………………………
………………………………………

**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

Ka katika "haijawa kutokea" , e na swali linalofu

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kumkataza mama kufanya kitu alichotaka kufanya baada ya kuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati alipokuwa akimkataza mama yangu kufanya kitu alichotaka kufanya**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimkataza mama yangu kufanya kitu alichotaka kufanya**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimkataza mama yangu kufanya kitu alichotaka kufanya**



4. Ni mara ngapi baba yako amemkataza mama yako kula au kulala, au kumfanya ashindwe kula au kulala?

| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea" , endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kumkataza mama yangu kula au kulala baada yakuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati alipokuwa akimkataza mama yangu kula au kulala**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimkataza mama yangu kula au kulala**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimkataza mama yangu kula au kulala**

***Tafadhali jua kwamba sio kosa lako ikitokea kuwa wazazi wako huwa wanagombana kuhusu wewe.***

5. Ni mara ngapi mama na baba yako wamewahi kugombana au kubishana kuhusu wewe?


| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea" , endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu na mama yangu wakigombana kuhusu mimi baada yakuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu na mama yangu wakati wakigombana kuhusu mimi**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akigombana na mama yangu kuhusu mimi**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akigombana na mama yangu kuhusu mimi**

6. Ni mara ngapi baba yako amevunja au kuharibu kitu kwa makusudi au akiwa na hasira? Kwa mfano: kupiga ukuta, kubamiza simu ukutani au sakafuni, au kuvunja kitu, kama vile vyombo.



**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea" , endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kuvunja kitu kwa makusudi au kwa hasira baada ya kuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati akivunja kitu**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akivunja kitu kwa makusudi au kwa hasira**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akivunja kitu kwa makusudi au kwa hasira**

7. Ni mara ngapi baba yako amefanya kitendo cha kumuumiza mwili mama yako, kama kumpiga kwa kitu kama mwiko, fimbo au mkanda, mateke, kumkaba au kuvuta nywele zake?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**


Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea" , endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kuumiza mwili wa mama yangu baada ya kuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati akimuumiza mama yangu mwili wake**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimuumiza mama yangu mwili wake**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimuumiza mama yangu mwili wake**

Kuna kitendo kingine chochote?
…………………………………………….

8. Ni mara ngapi baba yako amewahi **kumtishia** mama yako kutumia kisu, mkanda, panga au silaha nyingine?



**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea", endelea na swali linalofuata

**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu kumuumiza mama yangu kwa silaha baada yakuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati akimuumiza mama yangu kwa silaha**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimuumiza mama yangu kwa silaha**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimuumiza mama yangu kwa silaha**

9. Ni mara ngapi baba yako **amemuumiza** mama yako kwa kutumia kisu, mkanda, panga?

**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

Kama umeweka tiki katika chaguo la "haijawahi kutokea", endelea na swali linalofuata


**Ulijuaje?**

- ☐ **Niliona matokeo yake (kwa mfano kuna mtu aliumia, kuna kitu kilivunjika, au kuna mtu alikuja kuwaamulia)**
- ☐ **Nilisikia kuhusu baba yangu akimtishia mama yangu kwa silaha baada yakuwa imeshatokea.**
- ☐ **Nilimsikia baba yangu wakati akimtishia mama yangu kwa silaha**
- ☐ **Nilimuona kwa mbali baba yangu alipokuwa akimtishia mama yangu kwa silaha**
- ☐ **Nilimshuhudia baba yangu kwa karibu wakati alipokuwa akimtishia mama yangu kwa silaha**

**<u>Sehemu ya pili</u>**

**Ni vigumu sana kujua nini cha kufanya unapoona mtu kafanyiwa kitu ili ajisikie vibaya, kwa mfano mtu anapokuwa na mawazo mengi sana. Maswali katika sehemu hii yanahusu mama yako kufanyiwa mambo mabaya yanayomfanya ajisikie vibaya, baba yako kutishia kumuumiza mama yako lakini hafanyi hivyo, au mwili wa mama yako kuumizwa, au mama yako kukatazwa kufanya kitu fulani.**

**Chagua jibu linaloendana na hali yako na uweke tiki. Jibu lolote utakalochagua litakuwa sahihi.**



10. Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi umepiga mayowe na kuwalilia ukiwa katika **chumba kingine tofauti** na kile ambacho ugomvi unaendelea?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

11. Ni Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi umewahi kuwapigia mayowe huku ukiwa katika **chumba ambacho ugomvi unaendelea**?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

12. Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi umemwita mtu mkubwa ili akusaidie kwa mfano, kumwita ndugu au jirani?


**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

13. Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi umeingilia ugomvi wao ili kujaribu kuwaamulia/kuwatenganisha wasigombane?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

14. Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi amekufanyia kitu wewe mfano kukupiga au kukutukana ili kumfanya mama yako aogope au ajisikie vibaya?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**



15. Wakati baba yako anapokuwa akimuumiza mama yako, ni mara ngapi umejaribu kuwa mbali na ugomvi wao kwa: kujificha, kuondoka nyumbani au kujifungia katika chumba kingine?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

Taja kitu kingine ambacho huwa unafanya kuwa mbali na ugomvi wao ……………….
………………………………………………

**16.** Ni mara Ni mara ngapi baba yako amekuomba umwambia kile ambacho mama yako amekuwa akifanya au kusema?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

17. Ni mara ngapi umekuwa na wasiwasi kuhusu **baba** yako kulewa au kutumia madawa ya kulevya?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

18. Ni mara ngapi umekuwa na wasiwasi kuhusu **mama** yako kulewa au kutumia madawa ya kulevya?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**


19. Ni mara ngapi mama yako ameonekana kukosa raha, mwenye wasiwasi au huzuni?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

20. Ni mara ngapi imeonekana kama kumekuwa na mabadiliko makubwa katika maisha yako? Kwa mfano: Kuhama nyumba, kulazwa hospitali kwaajili ya matibabu, wazazi kutarakiana (wazazi kutengana) kifo cha mtu wako wa karibu sana au mzazi kufungwa gerezani?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

- Taja mabadiliko mengine makubwa yaliyotokea katika maisha yako ……………………………..….



21. Ni mara ngapi umewahi kusikia majirani zako, mtaani au shuleni kwenu mtu fulani akimfanya mtu mwingine ajisikie vibaya kwa kumtania, kumwambia maneno mabaya au machafu?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

22. Ni mara ngapi jirani yako yeyote, mtu mtaani kwako au shuleni kwenu amekutania au kukuambia maneno mabaya au machafu ili kukufanya ujisikie vibaya?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

23. Ni mara ngapi umemuumiza mtu kwa makusudi kwa kumtania, kumwambia maneno mabaya au machafu?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

24. Ni mara ngapi umeumiza mwili wa mtu kwa makusudi kwa mfano kumrushia ngumi au kumpiga mateke?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

25. Ni mara ngapi umewahi kumwona jirani au mtu yeyote mtaani au shuleni kwenu akiumizwa kwa: kukabwa, kupigwa vibao, mateke au kuumizwa kwa kutumia silaha kwa mfano kisu, panga au mkanda?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

- Taja namna nyingine ya kumuumiza mtu ambayo umeiona kwa majirani, mtaani au shuleni kwenu………………………..


26. Ni mara ngapi mtu wa shuleni au mtaani kwenu amewahi kukuumiza kwa: kukukaba, kukupiga vibao, mateke au kukuumiza kwa kutumia silaha kwa mfano kisu, panga au mkanda?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**

- Taja namna nyingine uliyowahi kuumizwa na mtu shuleni au mtaani kwenu...............

27. Ni mara ngapi umewahi kuona mtu akiumizwa au kuuliwa katika TV (televisheni) au filamu?

**Haijawahi kutokea** **Mara chache** **Mara nyingi** **Kila siku**



28. Ni mara ngapi umewahi kuona mtu akiumizwa au kuuliwa kwenye gemu za kuchezea kwa rimoti, kwenye simu, kwenye TV au kwenye kompyuta?

| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

29. Ni mara ngapi mtu mzima katika familia yenu ameumiza hisia zako au amekufanya ujisikie vibaya kwa: kukutania, kukuambia maneno mabaya au machafu, au kukutishia kukuumiza?

| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

Taja vitu vingine vinavyokuumiza hisia zako au kukufanya ujisikie vibaya…………………………………………..

30. Ni mara ngapi mtu mkubwa katika familia yenu kaumiza mwili wako kwa mfano kukupiga vibao, kukupiga mateke au kukuchapa kwa fimbo?

| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

- Taja namna nyingine yoyote ambayo mtu mkubwa katika familia yenu kakuumiza mwili wako


………………………………

***Tungependa kujua mambo yanayowapata watoto yawe mazuri au mabaya. Wakati mwingine watoto wanafanya mambo na wasijue kuwa ni mabaya, au wanalazimishwa kuyafanya. Kwa maswali yafuatayo, naomba uniambie kile ambacho huwa kinatokea. Utakachoniambia ni kwa ajili tu ya kujua unayopitia.***

***31.*** Ni mara ngapi mtu ambaye si wa familia yenu amegusa sehemu zako za siri bila ruhusa yako, amekulazimisha kugusa sehemu zake za siri, amekulazimisha kimapenzi au kufanya nae ngono?

| Haijawahi kutokea | Mara chache | Mara nyingi | Kila siku |
|---|---|---|---|

32. Ni mara ngapi mtu yeyote katika familia yenu awe mwanamke au mwanaume, amewahi kugusa sehemu zako za siri bila ruhusa yako, amekulazimisha kugusa sehemu zake za siri, amekulazimisha kimapenzi au kufanya nae ngono?



**Haijawahi kutokea** | **Mara chache** | **Mara nyingi** | **Kila siku**

## Sehemu ya tatu

33. Ikitokea baba na mama yako wanagombana au kufokeana ugomvi wao ulianza lini? (Weka tiki kwenye chaguo moja)

    i. Sikumbuki kama wamewahi kugombana
    ii. Walianza kugombana mwaka huu.
    iii. Walianza kugombana tangu nilipokuwa darasa la…………………………..
    iv. Wamekuwa wakigombana kwa muda mrefu kiasi kwamba siwezi kukumbuka ni lini walianza kugombana
    v. Haijawahi kutokea

34. Unafikiri familia yenu ina pesa za kutosha kwa ajili ya mahitaji yako? (Weka tiki kwenye chaguo moja)
    i. Hapana, kuna wakati familia yetu inakosa pesa kwaajili ya chakula, kodi ya nyumba au kwaajili ya mahitaji mengine.
    ii. Naona tuna pesa za kutosha kwa ajili ya mahitaji yetu.
    iii. Tuna pesa za kutosha kununua vitu vya ziada ambavyo wakati mwingine tunakuwa hata hatuvihitaji.
    iv. Sijui.

35. Una miaka mingapi? ……………………………..

36. Wewe ni mvulana au msichana? (Weka tiki kwenye chaguo moja).
    i. Mvulana
    ii. Msichana

37. Ulilala wapi usiku wa jana? (Weka tiki kwenye chaguo moja)
    Nililala:
    i. Kwenye nyumba tuliyojenga wenyewe (chumbani)
    ii. Kwenye nyumba ya kupanga
    iii. Sehemu maalumu kwa mfano kituo cha watoto yatima, shule ya bweni n.k
    iv. Taja sehemu nyingine ulipolala ………………………………………….

38. Unaishi wapi? (Weka tiki kwenye chaguo moja). Ninaishi:

i. Nyumbani na ndugu zangu
ii. Sehemu maalumu kwa mfano kituo cha watoto yatima, shule ya bweni n.k
iii. Taja sehemu nyingine unapoishi……………………………………….

39. Unaishi na nani? Tiki majibu yote yaliyo sahihi.

| | | |
|---|---|---|
| i. Mama | | vii. Mdogo wangu wa kiume (wadogo zangu wa kiume) |
| ii. Baba | | viii. Kaka yangu (kaka zangu) |
| iii Mama wa kambo | | ix. Mdogo wangu wa kike (wadogo zangu wa kike) |
| iv. Baba wa kambo | | x. Dada yangu (dada zangu) |
| v. Bibi | vi. Babu | xi. Taja mtu mwingine yeyote unayeishi nae ambaye hakutajwa hapo juu..………………………… |

40. Unapenda kufanya kazi gani za nyumbani? ...................................................